# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



# Utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025

# Yaliyomo

- Utangulizi
- Utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa Sekta

1. Sekta ya Kilimo
2. Sekta ya Mifugo na Uvuvi
3. Sekta ya Utalii
4. Sekta ya viwanda na biashara
5. Sekta ya Afya
6. Elimu
7. Maendeleo ya jamii
8. Mapato

# Utangulizi

- Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kama zilivyo taasisi zingine nchini inaendelea na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 kwa kuhakikisha inasimamia ipasavyo matumizi ya fedha zinazotolewa na Serikali pamoja na Wadau mbalimbali wa maendeleo kwa lengo la kuwatea maendeleo Wananchi wa Rungwe na Tanzania kwa ujumla. Fedha hizi ni pamoja na zinazoletwa kwa ajili kufadhili miradi mbalimbali ya kisekta kama vile elimu na afya.


# Utangulizi unaendelea…..

RUNGWE DISTRICT COUNCIL

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya wilaya ya Rungwe imepoke a fedha jumla ya kiasi cha **shilingi 6,279,179,328.63** Kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka sekta za Afya, Elimu, Maendeleo ya Jamii pamoja na Kilimo na mifugo.

Katika kuhakikisha Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 inatekelezwa kikamilifu, Halmashauri imejiwekea utaratibu Madhubuti wa kusimamia miradi inayotekelezwa ili miradi hiyo iakisi thamani halisi ya fedha iliyotolewa

# Bar chati kwa mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo. 2023/24




11 June 2025

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI KISEKTA

- Wilaya ya Rungwe kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo inatekeleza malengo na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa kuzingatia, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025
- Halmashauri imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya Maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu kwa sekta mbalimbali kama ifuatavyo;

# 1. SEKTA YA KILIMO

**Kukuza sekta ya kilimo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 ibara ya 37**

- Halmashauri ya wilaya ya Rungwe ina ukubwa wa hekta 123,186.00 na eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 92,390.6
- Kutokana na hali nzuri ya hewa, Sekta ya Kilimo inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Wilaya. Zaidi ya asilimia 90
- Mazao muhimu ya biashara ni Kahawa, Chai, Kokoa na Parachichi. Na mazao ya chakula ni pamoja na Ndizi, Mahindi, Viazi mviringo, Viazi vitamu, Maharage na Mpunga.

## Sekta ya Kilimo inaendelea…

**Mafanikio ya sekta ya kilimo**

- Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula ambapo Halmashauri inajitosheleza kwa chakula na ziada inauzwa nje ya Wilaya, Mkoa na Nchi jirani.
- Uzalishaji wa mazao ya biashara kama vile kahawa umeongezeka kutoka tani 647.7 mwaka 2020 hadi tani 1,226.5 Disemba 2024 sawa na ongezeko la asilimia 89.3
- Jumla vitalu 35 vya miche bora ya Parachichi, Kahawa na Kakao vimeanzishwa katika Kata za Bulyaga, Kyimo, Mpuguso Masukulu, Ikuti, Makandana, Lufingo na Kiwira

# Mafanikio Sekta ya Kilimo……….

- Ambapo vitalu 2 kati ya vitalu 35 vya parachichi na kakao vimeanzishwa na Halamashauri ya Rungwe na Vitalu viwili vya miche ya kahawa vilianzishwa na Bodi ya kahawa Tanzania na miche hiyo itagawiwa bure kwa wakulima.





# Sekta ya kilimo

- Jumla ya tani 6,537.8 **ya mbolea** za kupandia na kukuzia zimesambazwa na kununuliwa na wakulima na kupelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao. Jumla ya wakulima 39,650 Wamesajiliwa katika mfumo wa mbolea za ruzuku.

  Wastani wa uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kama ifuatavyo:-

  ***Mahindi*** tani 102,945 mwaka 2020 hadi tani 103,990 Disemba, 2024

- ***Ndizi tani*** 352,848 mwaka 2020 hadi tani 356,404.0 mwaka 2024
- Mpunga tani **3,023.0** mwaka 2020 hadi kufikia tani **3,080.5** kufikia Disemba, 2024.

## KILIMO MAFANIKIO……..

- Viazi mviringo tani **503,119.0** mwaka 2020 kufikia tani **503, 622** mwaka 2024
- Magimbi tani **7,820** mwaka **2020** kufikia tani **7,826.10** mwaka 2024
- ***Aidha***, Barabara yenye km 11 Ndulilo - Itete imejengwa kwa programe Agri-connect
- Wakulima wanaopata huduma za ugani wameongezeka kutoka Wakulima 66,387 mwaka 2020 na kufikia 75,105 Disemba, 2024

  Uwiano wa wakulima wanaotumia mbolea za viwandani umeongezeka kutoka 76% mwaka 2020 kufikia 87% kufikia 2024.
- Upimaji wa afya ya udongo, jumla ya sampuli 499 zimekusanywa, kupimwa na kutolewa matokeo kwa ajili ya kuwashauri wakulima kuanzia mwezi Julai hadi Disemba,2024.

# Upimaji wa udongo

- Jumla wakulima 249 walipimiwa sampuli na kupewa ushauri wa aina na kiasi cha mbolea wanachopaswa kutumia katika mashamba yao.

# KILIMO……. Ushirika



- Mitaji katika vyama vya Ushirika imeongezeka kutokana na uhamasishaji na uanzishwaji wa vyama viwili vya Ushirika vya zao la parachichi na mboga mboga na matunda kwa kufikia Sh 739,197,091 mwaka 2024 kutoka Kiasi kilichokuwepo cha Sh.728,696,891 mwaka 2020
- Uzalishaji wa zao la kokoa umeongezeka kupitia vyama vya Ushirika kutoka Tani 581 mwaka 2020/2021 na kufikia Tani 758 mwaka 2023/2024
- Uzalishaji wa zao la kahawa kupitia vyama vya Ushirika umeongezeka kutoka Tani 627 mwaka 2020/2021 na kufikia Tani 1,758 mwaka 2023/2024

# KILIMO…….

- Vyama vya Ushirika 102 vimeanza kutumia mfumo mpya wa usimamizi wa kidigitali uitwao MUVU kwa mwaka 2024/2025 hasa katika kuboresha na kutunza kumbukumbu za chama na wanachama.
- Utunzaji huu wa kumbukumbu utasaidia katika kubaini changamoto na pia katika ukaguzi wa hesabu za vyama vya Ushirika.
- Vyama Vya Ushirika 102 kati ya vyama 109 vimeweza kukaguliwa na ofisi ya Ushirika na Wakaguzi wa Nje waitwao COASCO na hali ilivyo kwa sasa ukaguzi uliofanywa umesaidia utendaji wa vyama kuendelea kuimarika.

## Sekta ya Kilimo …Changamoto

- Kushuka kwa baadhi ya mazao ya biashara Kutokana na kutopatikana kwa pembejeo kwa wakati
- Ukosefu wa uhakika wa masoko ya mazao
- Bei ndogo za mazao ya kilimo ikilinganishwa na gharama za uzalishaji
- Vyama vingi bado havijaajiri watendaji wenye sifa stahiki katika kusimamia na uendeshwaji wa Vyama.

## Sekta ya Mifugo

- Wakazi wa Rungwe hufuga mifugo mbalimbali hasa ng’ombe, mbuzi kondoo, nguruwe, kuku. Kwa takwimu zifuatazo

| Aina ya Mfugo | Mwaka 2023 | Disemba 2024 |
|---|---|---|
| 1. Ng’ombe | 49,790 | 52,208 |
| 2. Mbuzi | 2,800 | 3,852 |
| 3. Kondoo | 270 | 350 |
| 4. Kuku | 219,277 | 455,866 |
| 5. Nguruwe | 16,709 | 40,022 |

- Aidha, Kuendelea kuenea kwa ng’ombe bora wa kisasa kumechangiwa na upandishaji ng’ombe kwa njia ya chupa (Uhimilishaji) 2024/2025.

## Sekta ya Mifugo inaendelea……

- Takwimu za mwaka 2024/2025 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa upande wa ng'ombe wa kisasa.

| Mwaka | Idadi ya Ng'ombe | Uzalishaji wa Maziwa (lita) |
| --- | --- | --- |
| 2020 | 41,166 | 48,339,708 |
| 2024 | 44,717 | 64,800,000 |

- **lita 64,800,000** kwa mwaka ni sawa na wastani wa **lita 180,000** kwa siku na wastani wa uzalishaji kwa ng'ombe mmoja kwa siku ni lita 10 hadi 15.
- Kiasi kinachouzwa kwenye soko rasmi ni **Lita 33,100** kwa siku sawa na 18% ambapo Kampuni ya ASAS Dairy Company inanunua kiasi cha **lita 28,000** kwa siku. Na kiasi kikubwa cha maziwa huuzwa kwenye soko lisilo rasmi

# MIFUGO… MAFANIKIO



## Ufugaji wa Samaki

- Ongezeko la mavuno ya samaki aina ya Pelege kutoka kg 3,291.5 mwaka 2020 kufikia kg 6,730 mwaka 2024 yenye thamani ya Shilingi 60,570,000 kwa mwaka wa fedha 2023/2024
- Kuongezeka idadi ya mabwawa ya ufugaji wa samaki kutoka 250 mwaka 2020 hadi kufikia 304 Disemba, 2024

## Sekta ya Mifugo ……

- **Changamoto** zinazoikabili sekta hii ya Kilimo ni pamoja na:
  1. Upatikanaji wa soko la maziwa lenye tija kwa mfugaji
  2. Upungufu wa maafisa ugani. Kwa sasa Halmashauri ina upungufu wa maafisa ugani 69.
  3. Uchakavu wa miundo mbinu ya machinjio

# Sekta ya mifugo…..

## Utatuzi wa changamoto

- Halmashauri inaendelea kuwashawishi wajasiriamali kuendelea kuwekeza katika biashara ya maziwa ambapo kwa mwaka 2023/2024 mafunzo kwa wajasiliamali 108 yametolewa juu ya namna bora ya kusindika maziwa kwa kata za Ibighi, Bagamoyo , Kyimo na Kiwira.
- Kampuni ya ASAS imejenga Kiwanda na kuanza majaribio ya kusindika Maziwa chenye uwezo wa Kusindika lita 50,000 kwa siku.
- Watumishi 20 wameajiriwa mwaka wa fedha, 2023/2024 na kufanya jumla ya watumishi kuwa 43, kutoka watumishi 23 walikuwepo mwaka 2020/2021

# KIWANDA CHA MAZIWA ASAS

11 June 2025



# VIVUTIO VYA UTALII  RUNGWE






# SEKTA YA UTALII


**Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020 – 2025 ibara ya 71 inaelekeza kuhakikisha tunakuza sekta ya utalii ili kukuza pato la Serikali**

**Halmashauri ya wilaya Rungwe ni moja kati ya maeneo machache hapa nchini yenye vivutio vingi vya kitalii ambavyo ni vya kipekee.**

**Baadhi ya vivutio hivyo ni**

- Hifadhi Asilia ya Mlima Rungwe,
- Maporomoko ya Maji (Kapologwe,Malasusa,Malamba
- Daraja la Mungu, Kijungu,
- Maziwa ya Volkano (Ngosi,Kisiba,Ndwati n.k),
- Majengo ya kale,
- Nyumba ya kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
- *Pamoja na maeneo mengi yenye fursa za uwekezaji na yanayovutia hisia za watu.*









# Fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii

- Makampuni ya kitalii
- Makampuni ya usafirishaji ( travel agencies)
- Biashara ya Utalii wa kitamaduni( bidhaa za asili, ngoma za asili, vyakula, mavazi nk)
- Kambi za kitalii, hoteli, migahawa ya kitalii
- Kuandaa filamu, picha za kibiashara n.k
- Vikundi vya waongoza watalii (tour guides)

# SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

**Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 ibara ya 32 na 46 inaelekeza kuhakikisha tunakuza sekta ya viwanda na biashara**



- Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina viwanda Vidogo, vya Kati na Vikubwa ambavyo vinajishughulisha na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo na uvuvi.
- Kuna jumla ya viwanda vidogo 124 vikijishughulisha na usagaji wa unga, ufundi seremala na ushonaji
- Viwanda vya kati 6 na
- Viwanda vikubwa sita (5) ambavyo vinajishughulisha na Gesi ya asili na usindikaji wa mazao ya vyakula

# BIASHARA

- Wilaya ya Rungwe kama Wilaya zingine za Mkoa wa Mbeya inao wafanyabiashara ambao hutoa huduma za mahitaji mbalimbali yatokanayo na viwanda na kilimo kwa wananchi.
- Idara imefanikiwa kusimamia utengaji wa maeneo ya wafanyabiashara wadogo na kuwapanga katika maeneo hayo kutoka katika maeneo yasiyo rasmi waliyokuwa wakifanyia biashara. Kwa kuwahamishia maeneo salama Tandale Sokoni.

# BIASHARA



Mkakati wa Halmashauri ni

- kuboresha vituo vya kufanyia biashara vilivyopo na kutafuta masoko mapya ikiwa ni muendelezo wa uboreshaji wa masoko ya Tandale, Machinga Garden" ili kumsaidia mzalishaji hasa wa mazao ya Kilimo na Mifugo kuuza kwa bei nzuri ambayo itamuongezea kipato.

# SEKTA YA AFYA

**Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 ibara ya 83, 84, 86, 88 na 91 inaelekeza kuhakikisha tunaboresha mazingira ya utoaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya.**

- **Miundombinu ya Afya.**
  - Halmashauri in jumla ya hospitali 1, Ongezeko la Zahanati 4 kutoka Zahanati 37 mwaka 2020 hadi kufikia 41 Disemba, 2024.
  - Kuongezeka kwa vituo vya Afya 7 mwaka 2020 hadi kufikia vituo vya Afya 9 Disemba 2024.

**Huduma za Mama na Mtoto**

- Vifo vya wajawazito vimepungua kutoka wastani wa vifo 60/100,000 mwaka 2023 hadi vifo 23/100,000 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa kitaifa 454/100,000

# Afya inaendelea…

- Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 22/1,000 mwaka 2021 hadi vifo 13/1,000 mwaka 2022 ikilinanisVwa na wastani wa kitaifa 17/1,000

**Magonjwa ya Mlipuko.**

- Kwa kipindi cha miaka mitano Halmashauri imefanikiwa kudhibiti magonjwa ya Milipuko ukiwepo ugonjwa wa Kipindupindu na UVIKO 19.
- Hadi Disemba, 2024 hali ya upatikanaji wa Dawa na vifaa tiba ni asilimia 92.

# Afya inaendelea…



- Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri imfanikiwa kufungua kitua kimoja cha Afya Kinyala na kuendelea na ujenzi wa vituo viwili ya afya Kata za Kiwira na Masoko.
- Aidha Halmashauri imeendelea na ujenzi wa zahanati za Kyosa hadi kufikia Disemba ujenzi umekamilika, na Matwebe ujenzi unaendelea.

# Kituo cha afya kata ya kinyala



# Kituo cha afya kiwira



# KITUO CHA AFYA IPONJOLA



# Elimu ya Msingi



**Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 ibara ya 80 inaelekeza kuhakikisha tunaboresha mazingira ya kutolea huduma ya elimu.**

| Idadi ya Shule za Msingi | | Shule mpya | Jumla |
|---|---|---|---|
| Serikali | **142** | **05** | **147** |
| Binafsi | **10** | **-** | **10** |

- Zenye wanafunzi 58,811 wakiwemo wavulana 29,278 na wasichana 29,533
- Vyumba vya madarasa vimeongezeka kutoka 1,011 mwaka 2020 hadi vyumba 1,157 hadi Disemba, 2024
- Ufaulu kwa darasa la saba umeongezeka kutoka 85.27% Mwaka 2020 kwenda 96.58% Mwaka 2024



SHULE YA MSINGI KIBUMBE

# ELIMU SEKONDARI

- Shule 07 za Sekondari zimejengwa ambazo ni Msasani, Lupepo, Kikota, Lukata, Isaka, Kyobo na Kibisi na kufanya kuwa na jumla ya shule za sekondari 39 za Serikali zenye wanafunzi 22,098 Wakiwemo wavulana 10,301 na wasichana 11,797
- Nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 92 in 2015 hadi kufikia 103 Disemba, 2024
- Kiwango cha ufaulu katika mtihani wa kidato cha Nne kimeongezeka kutoka 93.57% mwaka 2020 hadi 95.9% Disemba 2024
- Kiwango cha ufaulu kidato cha Sita kimeongezeka kutoka 99.5% mwaka 2021 kufikia 100% Juni 2024.

# MWONEKANO SHULE YA SEKONDARI LUPEPO.







# KISONDELA SEKONDARI

# Shule ya Sekondari NDEMBELA 1



# UJENZI WA MABWENI MAWILI SHULE YA SEKONDARI KAYUKI



11 June 2025

# UJENZI WA SHULE YA AMALI KISONDELA





# UJENZI WA SHULE MPYA YA KATA YA KAWETELE





# Maendeleo ya jamii

***Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 ibara za 26 na 229 inaelekeza kuhakikisha tunakuza utawi na maendeleo ya Wananchi***



Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imefanikiwa:

- Kupambana na kudhibiti kuenea kwa maambukizi mapya ya HIV/AIDs katika ngazi ya jamii kutoka 9.3% iliyokuwepo na kufikia 9.0% kufikia 2024.
- Kutekeleza na kusimamia miradi inayolenga kuondoa umasikini na kuboresha maisha ya wananachi katika makundi yote
- Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu imeongezeka kutoka shillingi **848,500,000.00** mwaka wa Fedha 2020/21 hadi kufikia shilingi **1,867,527,500.00** kwa mwaka Fedha 2023/24 Disemba 2024.

# Maendeleo ya jamii…….



- Katika mwaka wa Fedha 2022/23 Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo yenye jumla ya Shilingi 319,000,000.00 Kwa vikundi 24. Ambapo Wanawake ni vikundi 14 Vijana Vikundi 06 na Watu wenye Ulemavu vikundi 04.
- Aidha, mikopo ya 10% haijaendelea kutolewa kuanzia April, 2023 kutokana na tangazo la kusitisha mikopo hiyo la Mhe. Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzaia Kassimu Majaliwa Kasimu.

# Maendeleo ya jamii…….


- Hata hivyo, baada ya kuruhusiwa kuendelea kutoa mikopo, Halmashauri inatarajia kutoa mikopo yenye thamani ya Tshs. 632,500,000.00 kwa awamu ya kwanza kwa vikundi 65 vikiwemo vikundi vya wanawake 39 vikundi vya vijana 23 na vikundi 3 vya watu wenye ulemavu.

# Makusanyo ya mapato ya halmashauri



- Halmashauri imefanikiwa kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani kutoka 96% mwaka wa Fedha 2021/22 kufikia 103% mwaka wa fedha 2023/24
- Ongezeko la mapato ni kutokana na matumizi ya mfumo wa kukusanyia mapato wa TAUSI kwa kutumia POS umesaidia ongezeko la makusanyo na udhibiti wa Bajeti kwa ujumla wake
- Kuimarika kwa mfumo wa ukaguzi wa ndani
- Mfuma wa makusanyo ya kodi na malipo mbalimbali umeimarika.

# MRADI WA KIMKAKATI STENDI YA MABASI TUKUYU



# MAPATO YA NDANI



| MWENENDO WA MAPATO YA NDANI KWA MIAKA MIWILI | | | |
|---|---|---|---|
| **MWAKA** | MAKISIO | MAPATO | ASILIMIA YA MWAKA |
| **2022/2023** | 6,131,460,000.00 | 5,878,114,572.46 | 96 |
| **2023/2024** | 7,179,615,400.00 | 7,365,389,030.24 | 103 |

# Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa hadi sasa



Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kiasi cha shingi **8,737,485,047.79** Kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Elimu na Afya. Ifuatayo ni miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe;

## MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA HADI SASA



SEKTA YA AFYA

- Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje pamoja na wodi za Wanawake na Wanaume katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu
- Ujenzi wa kituo cha Afya katika kata ya Kiwira kwa gharama ya shilingi milioni 500
- Ujenzi wa kituo cha Afya katika kata ya Masoko shilingi milioni 500.

# Ujenzi wa jengo la OPD hospitali ya wilaya



# UJENZI WA OPD NA WODI MAKANDANA



# JENGO LA OPD HOSPITALI YA TUKUYU (MAKANDANA)



# SEKTA YA AFYA ………



- Ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vya Afya Kinyala, Kalebela na Iponjola na Ndanto kwa gharama ya shilingi milioni 600
- Ukamilishaji wa Zahanati za Isyonje na Ilenge kwa gharama ya shilingi milioni 100
- Ununuzi wa vifaa tiba katika zahanati za Ilenge, Kyosa,Nkunga na Swaya kwa gharama ya shilingi milioni 100

# UJENZI WA KITUO CHA AFYA MASOKO



# SEKTA YA ELIMU SEKONDARI



1. Ukamilishaji wa maabara 1 katika shule ya sekondari Kikota kwa gharama ya shilingi 30,000,000/= (Milioni Thelathini)
2. Ukamilishaji wa mabweni 2 Sekondari ya Kisondela na Lupoto kwa gharama ya Shilingi 83,155,967.89
3. Ujenzi wa vyumba 41 vya madarasa kwa gharama ya shilingi 580,400,000/= (Milioni mia tano themanini na laki nne tu) kwenye shule 9 kwa idadi tofauti tofauti za madarasa.

# SEKTA YA ELIMU SEKONDARI



Ujenzi wa Matundu 93 ya vyoo yenye gharama ya shilingi 147,000,000 /= (Milioni mia moja arobaini na saba )

kwenye shule 13 ambapo kila shule ilijenga matundu 8

Ujenzi wa nyumba 2 za Watumishi katika shule ya sekondari Kyobo na msasani za kuishi watumishi 4 (2:1) kwa gharama ya shilingi 214,000,000/= ( Milioni mia mbili kumi na nne)

# SEKTA YA ELIMU MSINGI



- Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa pamoja na matundu 12 ya vyoo katika shule ya msingi Umoja shule ya mchepuo wa Kiingereza kwa gharama ya shilingi **milioni 63**
- Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule ya msingi Lupoto na Ibungila kwa gharama ya shilingi **milioni 40**

# SEKTA YA ELIMU MSINGI ……….

- Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule ya msingi Mibula kwa shilingi **milioni 50**
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 34 katika shule za msingi Ibuka na Bunyangomale kwa gharama ya shilingi milioni **94.4**
- Ujenzi wa vyumba 9 vya madarasa pamoja na matundu 18 vyoo katika shule za msingi Bulyaga,Mabonde, Kigugu, Masebe, Mpunguti, Katumba I,Iponjola, Lupepo na Swaya kwa gharama ya shilingi **milioni 208**
- Ujenzi wa **Walk way** katika shule ya wanafunzi wa mhitaji Maalum kwa gharama ya Shilingi **milioni 30.**

# UKAMILISHAJI WA ZAHANATI YA KYOSA



# Utekelezaji wa miradi .. Muendelezo 2024

Aidha kwa mwaka 2024 hadi sasa kiasi cha **Shilingi 2,966,360,056** kimeshapokelewa kwa kuendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo.



| NA | JINA LA MRADI | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|
| | A. IDARA YA AFYA | |
| 1 | Ukamilishaji wa Ujenzi wa Ghorofa Hospitali ya wilaya | 700,000,000.00 |
| 2 | Ununuzi wa vifaa tiba Hospitali ya Wilaya | 300,000,000.00 |
| 3 | Ununuzi wa vifaa tiba Zahanati ya Bujela | 25,000,000.00 |
| 4 | Ununuzi wa Vifaa Tiba Zahanati Swaya. | 25,000,000.00 |
| 5 | Ununuzi wa vifaa tiba Zahanati ya Masoko | 50,000,000.00 |
| | B. IDARA YA ELIMU SEKONDARI | 1,100,000,000 |
| 1. | Kusaidia ujenzi wa Hostel Masoko Sekondari | 30,000,000.00 |
| 2. | Kusaidia ukamilishaji wa hostel Ikuti Sekondari | 30,000,000.00 |
| 3. | Ukamilishaji wa Boma la Bwalo Isongole Sekondari | 100,000,000.00 |
| 4. | Ukamilishaji wa Boma la Bwalo Kinyala Sekondari | 20,000,000.00 |
| | C. IDARA YA ELIMU MSINGI | 180,000,000.00 |

# Utekelezaji wa miradi .. Muendelezo 2024



MIRADI YA SHULE ZA SEKONDARI ITAKAYOTEKELEZWA KUPITIA PROGRAMU YA SECONDARI EDUCATION QUALITY IMPROVEMENT – (SEQUIP)

| Na. | JINA LA MRADI | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari Kata ya Kawetele | 583,180,028.00 |
| 2. | Ujenzi wa Shule Mpya ya Amali Kisondela | 583,180,028.00 |
| 3. | Ujenzi wa Nyumba ya Walimu 2/1, Mabweni 2 na vyumba 4 vya madasa Shule ya Sekondari Lupepo | 480,000,000.00 |
| 4. | Ujenzi wa mabweni 2 Shule ya Sekondari Kayuki | 260,000,000.00 |
| 5. | **JUMLA** | **1,906,360,056.00** |

# MAPOKEZI YA WATUMISHI WAPYA



- Halmashauri ya imepokea watumishi 170 wa kada za Afya na Utawala
- Afya 130
- Idara ya Utawala 40

Halmasahuri  ina jumla ya watumishi  3,327 na upungufu watumishi 747  katika kada za elimu, Afya,….

# SEKTA YA MAJI

- ***Kubuni na kutekeleza miradi ya maji katika vijiji na miji iliyopo katika mziwa makuu ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 ibara ya 100***
- Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini imetekeleza jumla ya miradi ya maji 11 kwa mwaka 2023/24 kwenye halmashauri ya Rungwe
- Miradi ambayo imeanza kutoa huduma ni 4 ambayo ni Ibililo,Lupepo-Mpombo,Ikuti-Lyenje na Ngopyolo

# SEKTA YA MAJI INAENDELEA………

- ***Kubuni na kutekeleza miradi ya maji katika vijiji na miji iliyopo katika mziwa makuu ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 ibara ya 100***
- Miradi inayoendelea kutekelezwa ni 5 ambayo ni ya Mradi wa Lupepo/Mpombo, Ikuti/lyenje,Masoko II pahase I,Ibililo,Ngopyolo ,.
- Sababu za kusimama,kuchelewa kukamilika ni mtiririko mdogo wa fedha. Aidha, RUWASA inaendelea kuikumbusha Wizara ya Maji kutuma fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati

## SEKTA YA MAJI INAENDELEA………

- ***Kendelea kukarabati na kujenga miundombinu mipya ya usambazaji maji ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 ibara ya 99***

- RUWASA inategemea kutekeleza miradi mipya 6 ambayo ni Masoko II phase II, Kikota, Kagwina, Ilundo, Ibungila na Kanyegele.
- Asilimia ya upatikanaji wa maji kwa Halmashauri ya Rungwe ni 76.7

## SEKTA YA UMEME

- Usambazaji Umeme katika vijij vyote na maeneo ya pembezoni mwa mji ( miji – vijiji – Peri Urbani areas ) Kukamilisha kupitia mpango wa Umeme vijijini pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango kabambe wa Umeme vijijini ( Rural Energy Master Plan) ***ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 ibara ya 63***
- Halmashauri ya wilaya ya Rungwe inapata umeme kutoka Grid ya Taifa kupitia kituo cha kupoozea umeme cha Mwakibete Mbeya kwenye laini ya msongo wa kilovoti 33

## SEKTA YA UMEME……..

- Matumizi ya juu ya Wilaya kwa sasa yanakadiriwa kuwa Megawati 8.
- Hali ya upatikanaji wa Umeme ni ya kuridhisha. Idadi ya watumiaji wa Umeme hadi sasa ni 40,014.

**Utekelezaji wa Miradi 2023/2024**

Miradi ina tekelezwa kwa aina mbili

- Miradi inayotekelezwa kupitia bajeti ya ndani ya Tanesco
- Miradi inayotekelezwa kupitia wakala wa umeme vijijini (REA)

**Miradi inayotekelezwa kwa Bajeti ya Ndani**

- Jumla ya miradi inayotekelezwa kupitia bajeti ya ndani ya Tanesco ni 19 katika maeneo tofauti ambapo miradi 17 tayari imekamilika wananchi wanapata huduma.

**Miradi inayo tekelezwa kupitia wakala wa umeme vijijini ni mitatu (3)**

1.Mradi wa REA awamu ya III mzunguko wa II

Mradi huu unapeleka umeme katika Vijiji 31 ambapo vijiji 29 vimewashwa na vijiji 2 kazi inaendelea.

# SEKTA YA UMEME………

**2. Mradi wa Ujazilizi 2(b)**

- Mradi huu unapeleka Umeme katika vitongoji 27 ambapo vitongoji vyote 27 tayari vimewashwa.

**3. Mradi mpya wa kupeleka umeme katika maeneo ya miji - vijiji (Peri-urbani)**

Mradi huu unapeleka umeme katika vitongoji 5, Vitongoji 4 tayari vimewashwa nakitongoji 1 kilichosalia mkandarsi anaendelea na kazi.

**MITANO TENA**

**Asanteni kwa kunisikiliza**